

TANGAZO LA KAZI (LINARUDIWA)

TANROADS SACCOS INATARAJIA KUAJIRI MENEJA WA CHAMA KULINGANA NA HADIDU REJEA ZIFUATAZO

1. KUHUSU TANROADS SACCOS

Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo TANROADS (TANROADS SACCOS LTD), kilianzishwa Novemba 2003 chini ya sheria ya Vyama vya ushirika Na 20 ya Mwaka 2003 na kurekebishwa Mwaka 2013. Chama hiki kilianzishwa kikiwa na madhumuni ya kusaidiana kuinua kipato cha wafanyakazi wa TANROADS walio katika ajira ya kudumu na wale walio katika ajira ya muda Maalum. Chama cha ushirika wa Akiba na Mikopo TANROADS SACCOS, kimendikishwa kwa No DSR 896 tarehe 27/07/2006 pia kimepata Namba ya Mlipa Kodi TIN No 135-448-397 mwaka 2018.

2. KUSUDI NA WIGO WA KAZI

Bodi ya TANROADS SACCOS inakusudia kuajiri Meneja mwenye uwezo, ujuzi na Uzoefu wa kutosha katika kusimamia na kuendesha shughuli zinazohusu Ushirika wa Akiba na Mikopo. Meneja/Katibu wa Chama atakuwa ndiye msimamizi wa shughuli zote za Chama za kila siku kulingana na miongozo itakayotolewa na Bodi na pia atakuwa Katibu wa Vikao vya Bodi na atawajibika kwa Bodi ya TANROADS SACCOS.

3. KAZI NA MAJUKUMU YA MENEJA

Majukumu ya Meneja wa chama yatakuwa kama ifuatavyo:-

- ❖ Kutekeleza na kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika na Kanuni zake, Sheria ya Hudua Ndogo za Fedha na Kanuni zake, Sera ya Maendeleo ya Ushirika, Masharti ya chama, Kanuni na Sera mbalimbali zilizowekwa kwa ajili ya kuongoza utekelezaji wa shughuli za chama;
- ❖ Kuhakikisha mifumo ya utendaji na utoaji taarifa ipo madhubuti na inawezesha mawasiliano;
- ❖ Kwa kushauriana na Wajumbe wa Bodi, kuandaa mpango mkakati, mpango biashara, bajeti ya mwaka na program ya utekelezaji;
- ❖ Kuhakikisha malengo na shabaha za chama zinafikiwa;
- ❖ Kushughulikia masuala yote yanayowahusu watumishi, hususan mafunzo na uendelezaji wa rasilimali watu;
- ❖ Kwa kushirikiana na Wajumbe wa Bodi, kukiwakilisha Chama katika shughuli na uingiaji wa mikataba;
- ❖ Kuhakikisha vitabu vya hesabu vinaandikwa na hesabu zinaandaliwa na kuwasilishwa kwa Wakaguzi kwa wakati;

- ❖ Kuhakikisha taarifa ya mapato na matumizi, mizania, na taarifa ya mikopo iliyochelewa zimeandaliwa kwa usahihi na wakati;
- ❖ Kutoa taarifa za menejimenti kwenye vikao vya Bodi ambazo zinaeleza hali ya kifedha ya Chama ikianisha mizania, hesabu ya mapato na matumizi, taarifa ya mikopo iliyochelewa, bajeti ya mwaka, mwenendo wa chama na uwiano wake;
- ❖ Kuidhinisha matumizi yaliyoko kwenye makisio kwa viwango vilivyowekwa na Bodi na kutia saini kwenye nyaraka zinaruhusu utoaji fedha za chama kwa kuzingatia ukomo ulioainishwa kwenye sera za chama;
- ❖ Kuisaidia Bodi kupanga viwango stahiki vya riba, ada na gharama nyingine kwa bidhaa na huduma zitakazotolewa;
- ❖ Kuisaidia Bodi katika kubainisha dhamana zinazokubalika na zinazoweza kutumika kudhamini mikopo;
- ❖ Kuhakikisha kuwa kuna ukwasi wa kutosha kukidhi mahitaji ya mikopo, uchukuaji wa akiba na gharama za uendeshaji;
- ❖ Kusimamia ufungwaji na uendeshwaji wa akaunti za chama;
- ❖ Kuajiri na kuwafukuza kazi watumishi walioko katika mamlaka yake, na baadae kuidhinishwa na bodi, kulipa stahili za watumishi kama zitakavyoidhinishwa na Mkutano Mkuu, kuwatuza na kuwapandisha vyeo watumishi au kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wakosaji kwa kuzingatia sera ya utumishi;
- ❖ Kutoa taarifa stahiki kwa mamlaka zinazohusika kwa muda muafaka;
- ❖ Kutekeleza mapendekezo yanayotolewa kwenye taarifa za Wakaguzi wa Ndani na wa Nje na taarifa za kiuchunguzi zinazotolewa na mamlaka husika; na
- ❖ Majukumu mengine kadri ya maelekezo ya Bodi.

4. ELIMU NA UJUZI

- ❖ Awe na elimu isiyopungua Shahada ya kwanza au Stashahada ya juu katika Uhasibu, Fedha, Utawala, Uongozi, Uchumi, Sheria, Biashara au Elimu inayofanana na hizo kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali. Mwenye vyeti vya kitaalam atapewa kipaumbele,
- ❖ Awe na uwezo wa kutumia kompyuta na mifumo mbalimbali ya kifedha,
- ❖ Awe na uwezo wa Kuwasiliana kwa Kuongea na kuandika kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza.
- ❖ Awe na uzoefu wa utumishi kwenye nafasi ya meneja wa SACCOS usiopungua miaka mitatu (3) au taasisi nyingine, za vyama vya ushirika zinazofanana na SACCOS.
- ❖ Awe na kumbukumbu nzuri za utendaji kazi kabla ya kujiunga na TANROADS SACCOS LTD,

- ❖ Awe na Umri usiopungua miaka 35 na usiozidi miaka 55
- ❖ Na sifa nyingine za ziada.

5. VIAMBATISHO

- ❖ Barua ya maombi yenye kubandikwa picha ndogo (*passport size*),
- ❖ Wasifu binafsi wa mwombaji (CV) uwe na Majina matatu ya wadhamini wawe, waajiliwa wa serikali au shirika linalotambulika (*Referees*).
- ❖ Nakala za vyeti vya taaluma, kidato cha nne, kidato cha sita kwa waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika,
- ❖ Nakala ya cheti cha kuzaliwa,
- ❖ Kitambulisho cha taifa au leseni ya udereva au pasi ya kusafiria (passport) na barua ya uthibitisho wa makazi kutoka Serikali za mitaa,
- ❖ Mshahara unaohitaji.

6. JINSI YA KUOMBA

Barua za maombi zielekezwe kwa;

MWENYEKITI WA BODI,
TANROADS SACCOS LTD,
S. L. P 11364,
DAR ES SALAAM

Barua za maombi ziandikwe kwa lugha ya Kiswahili na kuwasilishwa kwa Njia ya barua pepe katika anuani **zote mbili** zilizoonyeshwa hapa chini; yovita.ngongji@tanroads.go.tz na pamela.masome@tanroads.go.tz. Mwisho wa kuwasilisha maombi ya ajira ni **tarehe 09/07/ 2020 Saa 10 Jioni**.

Aidha, waombaji waliowasilisha maombi yao awali, hawaruhusiwi kuomba kwa mara nyingine.

**Imetolewa leo Tarehe 26/06/ 2020
MWENYEKITI TANROADS SACCOS**